

## MAMBO MBALIMBALI KUHUSU MNYAMA WA UDH-HIYA



يجوز أن يهدى المسلم لقريبه وجاره أو غيرها من الكفار شيئاً من الطعام أو الشراب أو نعومهم، ولو من الأضحية، وأن يتصدق عليهم ططعوا إن كانوا فقراء؛ صلة للرحم، وأداء حق الجوار، وتاليفاً للقلوب، قال الله تعالى: {وَإِنْ جَاهَكُمْ عَلَى أَنْ تُشْرِكُوا بِي مَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ فَلَا طُغْفُهُمَا وَصَاحِبُهُمَا فِي الدُّنْيَا مَعْرُوفًا وَأَتَيْتُكُمْ مِّنْ أَنَابِإِنَّمَا قَالَ: لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يَقْاتِلُوكُمْ فِي الْأَرْضِ وَمَنْ يُخْرِجُكُمْ مِّن دِيَارِكُمْ أَنْ تَسْرُؤُهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ} وقد ثبت أن النبي - أمر أماء بنت أبي بكر رض أن تصل أنها، وكانت كافية حينئذ، وأهدى عمر بن الخطاب رضي الله عنه حللاً لقرباب له كافر، ولم يثبت في الشريعة ما يمنع من ذلك، والأصل الإباحة، لكن لا يعطي الكفار من الركوة إلا المؤلفة قلوبهم.

س 2: اشتربت شاة لأضحى بما فولدت قبل الذبح بمدة بسيرة، فماذا أفعل بولدها؟ ج 2: الأضحية تعين بشرائها بنية الأضحية أو بتعينها، فإذا تعينت فولدت وقت ذبحها فاذبح ولدها تبعاً.

س 1: البادحة يطبخون الأضحية مع بعض بدون تقسيم، ثم يجتمعون عليها سوياً بصفة وليمة، وإني قلت لهم: قسموها أفضلي، فقالوا: كل واحد مننا عنده أضحية، وكل يوم نأكل ذبيحة عند واحد سوياً. هل يجوز تكسير عظامها أو لا؟ ج 1: يجوز للجماعية أن يذبح كل واحد منهم أضحية في يوم من أيام العيد: يوم الأضحى وثلاثة أيام بعده، وأن يكسرعوا عظامها، وأن يطبوخوها وياكلوها جميعاً دون تقسيم، كما يجوز لهم أن يقسموها ويوزعوها بينهم قبل طبخها أو بعده، ويتصدقوا منها.

س: هل يجوز للرجل أن يذبح ذبيحة عيد الأضحى وهي ليس مدفوع ثمنها، ثم تسدد بعد مدة؟ وجراكم الله خيراً. ج: يجوز ذبح الأضحية ولو تأخر دفع قيمتها عن ذبحها.

س 2: هل يجوز التلفظ بالنية مثلاً لو أردت أن أذبح أضحية لوالدي المتوفى، فأقول: اللهم إما أضحية والدي فلا، أم أى أعمل الحاجة بدون تلفظ وبكتفي؟ ج 2: النية محلها القلب، فيكتفي بما قصدته في قلبه، ولا يتلفظ بالنية، وعليه بالتسمية والتکبير عند الذبح؛ لما ثبت في الصحيحين عن أنس رض قال: «ضحي النبي صل بكشين ذبحهما بيده وسي وكبر» (1). «ولا مانع من أن تقول: اللهم إن هذه أضحية عن والدي، وليس هذا من التلفظ بالنية.

س 2: والدي أبكم وهو الذي يذبح لها الأضحية، هل أذكر اسم الله تعالى بدلاً عنه على الأضحية؟ ج 2: الأبكم يسمى على الذبيحة حسب استطاعته وحسب النية في قوله مع الإشارة، ويكتفي بذلك، ولا يجزي أن يسمى شخص آخر بدلاً عنه.

س 1: ما هو حكم الأضحية، وما هو الأفضل، هل تقسم لمن أطبخها أفضلي؟ علماً أن فيه بعض الناس يقول: إنه لا يجوز في الثالث الذي يتصدق به أن يطبوخه أو يكسر عظمه.

ج 1: الأضحية ستة كفاية، وقال بعض أهل العلم: هي فرض عين، والأمر في توزيعها مطبوعة أو غير مطبوعة واسع، وإنما المشروع فيها أن يأكل منها، وبهدي، وبتصدق.

المصدر: اللجنة الدائمة للبحوث العلمية والإفتاء

### JE INAFAA KUMPA KAFIRI NYAMA YA UDH-HIYA?

Inafaa kwa muislamu kumpa chochote katika vyakula au nguo na vinginevyo, ndugu yake wa karibu na jirani yake na wengineo katika makafiri ; hata pia nyama ya udh-hiya. Na inafaa kuwapa sadaka endapo watakuwa wahitaji ili kuunga undugu na kutekeleza haki ya ujirani, na kuunga mioyo yao katika uislamu. Amesema Allah Mtukufu (( Na endapo wazazi wawili watakulazimisha kunishirikisha mimi pamoja na usiyekuwa na elimu naye, basi usiwatii na **endelea kuishi nao duniani kwa wema** na ifuate njia ya wenyen kujisogea kwangu)) na akasema pia [[ Allah hajakuktazeni kuwafanya wala hawakutoeni katika miji yenu, hajakukatazeni kuwafanya wema na kuwafanya uadilifu; hakika Allah anawapenda wafanyao uadilifu ]] Na hakika imethibitika kwamba Mtume alimuamrisha Asmaa Bint Abiibakr Allah awaridhie amfanyie wema mama yake ambaye alikuwa kafiri wakati huo, na pia imethibitika kwamba Umar Allah amridhie alimpala kafiri zawadi ya joho lake. Na hajkuthibitika katika sheria ya uislamu dalili yenyen kuzuila hilo, na asili ni uhalali, lakini kafiri hapewi katika mafungu ya zaka ya mali isipokuwa wenyen kuungwa mioyo yao katika uislamu.

### SWALI

Nilinunua mbuzi wa udh-hiya akazaa kitambo kidogo cha muda kabla ya kumchinja, nini nifanye kwa mtoto wake?

### JIBU:

Mnyama wa udh-hiya anakuwa kateuliwa rasmi kwa ajili ya kuchinjwa udh-hiya pindi atakaponunuliwa kwa nia ya udh-hiya au kwa kumchagua (mionganii mwa wanyama unaowamiliiki) , hivyo basi, endapo atakuwa kateuliwa au kachaguliwa (kwa mojawapo ya njia hizo mbili) kisha akajifungua kabla ya kumchinja basi mchiniye pia mtoto wake, kwa sababu ya kuambatana na mama yake (katika hukumu moja).

### SWALI

Je inafaa mtu kuchinja mnyama wa udh-hiya ambaye bado hajalipa thamani yake (amemnunua kwa mkopo) kisha italipwa pesa baadaye (baada ya kumchinja)? Allah akulipeni kheri nyingi.

### JIBU:

Inafaa kumchinja mnyama wa udh-hiya hata kama thamani yake itachelewa kulipwa baada ya kumchinja.

### SWALI

Ni ipi hukumu ya kuchinja mnyama wa udh-hiya na kipi kilichokuwa bora, je tugawe nyama kabla ya kuzipika au kuzipika ndio bora zaidi ? Kwa kutambua kuwa baadhi ya watu wanasema kuwa haifai kupika wala kukata mfupa wa theluthi ya nyama itakiwayo kutolewa sadaka ?

### JAWABU:

Kuchinja mnyama wa udh-hiya ni sunna yenye kutosheleza (wale waliookusanya katika nia ya mchinjaji) na baadhi ya wanazuoni wanasema ni Wajibu kwa kila mmoja kuchinja (isipokuwa asiyé na uwezo). Na jambo la kugawa nyama ya udh-hiya ikiwa imepikwa au ikiwa haijapikwa ni jambo lenye upana (yaani ana hiari kugawa ikiwa imepikwa au ikiwa mbichi), na jambo la msingi kisheria ni kula katika sehemu ya nyama hiyo, na kutoa zawadi na kutoa sadaka (katika sehemu ya nyama iliyobaki).

### SWALI:

Je inafaa kutamka nia , mathalani nikihitaji kuchinja mnyama wa udh-hiya kwa ajili ya mzazi wangu ali-yefariki nikasema ; "Ewe Allah huyu ni mnyama wa udh-hiya kwa ajili ya baba yangu fulani" au nitafanya hitajio langu pasina kutamka nia na inatosha?

### JAWABU:

Nia sehemu yake ni moyoni, linatosha kusudio ambalo limekusudiwa ndani ya moyo wake, wala asitamke nia bali anatakiwa aseme "Bismillah" kisha aseme "Allaahu Akbar" wakati wa kuchinja kama ilivyothibitika ndani ya Bukhari na Muslim, masimulizi kutoka kwa Anas Allah amridhie amesema "Mtume ﷺ alichinja kondoo wawili kwa mkono wake, alisema Bismillah kisha akasema Allaahu Akbar ]. Lakini hakuna katazo ikiwa utasema : ' Ewe Allah hakika huyu mnyama wa udh-hiya ni kwa ajili ya baba yangu' ; lakini matamko hayo si nia.

### SWALI

Watu wa vijiji ni huwa wanapika nyama ya udh-hiyah pamoja na wengine pasina kugawa nyama hiyo, kisha (wakati wa kula) wanakusanyika kwa pamoja kama vile walima, nami niliwaambia kuwa ; gawaneni nyama hiyo ndio jambo bora zaidi: wakasema "kila mmoja katika sisi ana mnyama wa udh-hiya na huwa tunakula kichinjwa cha udh-hiya kwa kukusanya pamoja kwa mmoja katika sisi (Je jambo hilo linafaa)? Na je, kuvunja mfupa wa mnyama wa udh-hiya inafaa au haifai ?

### JAWABU:

Inafaa kwa kikundi cha watu, kila mmoja katika wao akachinja mnyama wa udh-hiya katika siku mionganii mwa masiku ya sikukuu (Tarehe 10 Dhul-hijjah) na masiku matatu baada yake (tarehe 11,12 na 13). Na inafaa kukata mifupa ya mnyama wa udh-hiya, na inafaa kupoika kwa pamoja na kula kwa pamoja pasina kugawana; kama ambavyo inavyofaa pia kugawana baina yao kabla ya kuipika au baada ya kuipika , na kutoa sadaka sehemu fulani katika nyama hiyo.

### SWALI:

Baba yangu ni bubu, naye ndiye anatuchinjia mnyama wa udh-hiya, je nitaje jina la Allah (Bismillah) badala yake wakati wa kuchinja?

### JIBU;

Bubu atasema Bismillah wakati wa kuchinja mnyama kadiri ya uwezo na kwa mujibu wa nia ndani ya moyo wake pamoja na kuashiria, na hilo linatosha kwake. Wala haifai mtu mwagine atamke Bismillah badala yake.

وصلى الله على مُحَمَّدٍ وآلِهِ وصَحْبِهِ وَسَلَّمَ